# KCPE PREDICTION 2020

# KISWAHILI

***Soma kifungu kifuatavyo. Kina nafasi 1-15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne chagua jibu linalofaa zaidi.***

Mtu mmoja __1__ kwa __2__ mkuki na __3__ watatu wakajeruhiwa kufuatia mapigano __4__ kati ya wanakijiji __5__ sehemu __6__ Mbiu, kata __7__ ya Uraibu, eneo __8__ Maozo. Baadhi ya vifo hivyo vilisababishwa na __9__ wa pombe __10__

Polisi wa __11__ wakiongozwa na naibu __12__ chifu wa lokesheni __13__ walikuwa __14__ washukiwa na __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. aliuwawa | B. alilala | C. aliuawa | D. alikufisha |
| **2.** | A. kuchomwa | B. kuchomewa | C. kuwekwa | D. kuchomolewa |
| **3.** | A. mengine | B. wengine | C. mwengine | D. nyingine |
| **4.** | A. kali | B. mkali | C. wakali | D. makali |
| **5.** | A. wa | B. la | C. ya | D. na |
| **6.** | A. iitwayo | B. kiitwayo | C. liitwayo | D. iitwacho |
| **7.** | A. mdogo | B. kidogo | C. ndogo | D. dogo |
| **8.** | A. ya | B. la | C. za | D. wa |
| **9.** | A. wakunywaji | B. wanywaji | C. wakunywao | D. wakulao |
| **10.** | A. halali | B. haramu | C. hariri | D. halili |
| **11.** | A. haki | B. nchi | C. usalama | D. salama |
| **12.** | A. la | B. cha | C. za | D. wa |
| **13.** | A. hiyo | B. hio | C. hilo | D. hicho |
| **14.** | A. wakiwasuka | B. wakiwasaka | C. wakiwafuata | D. wakiwataka |
| **15.** | A. wahadhiri | B. wahunzi | C. wagema | D. walafi |

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**<u>Kutoka swati la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.</u>**

**16.** Ni neno lipi lenye silabi changamano?

A. Maisha

B. Kaka

C. Kiti

D. Ugonjwa

**17.** ________ ni mtaalamu wa kuunganisha viungo vya mwili vilivyovunjika.

A. Mhazili

B. Mualisaji

C. Mhazigi

D. Nesi

**18.** Watoto walicheza <u>vizuri</u> wakapewa zawadi <u>nzuri</u>. Tambua maneno yaliyopigwa mstari.

A. kielezi. kivumishi

B. kivumishi, kielezi

C. kielezi, kielezi

D. kivumishi, kivumishi

**19.** ***'Alimliza mtoto wa jirani'***, sentensi hii imenyambuliwa katika kauli gani?

A. Kutendeana

B. Kutendea

C. Kutendeshwa

D. Kutendesha

**20. Andika usemi halisi wa:-**

Mandila alisema kwamba angesafiri mwaka ambao ungefuata.

A. "Atasafiri mwaka ujao," Mandila alisema

B. "Nitasafiri mwaka ujao," Mandila alisema.

C. Alisafiri mwaka utakaofuata Mandila alisema.

D. Angesafiri mwaka uliopita Mandila alisema.

**21.** Chagua sentensi iliyoakifishwa vizuri.

A. Salima alinunua vitabu, viatu na begi

B. Salima alinunua: begi, vitabu na viatu.

C. Salima alinunua; viatu, begi, vitabu

D. Salima alinunua; begi na viatu na vitabu

**22. Ni methali ipi iliyo na maana sawa na:-**

Mvumilivu hula mbivu

A. Subira huvuta heri.

B. Haraka haraka haina baraka.

C. Bidii ya mja haiondoi kudura.

D. Ngoja ngoja huumiza matumbo.

**23.** Unda nomino kutokana na kitenzi imba.

A. imbia

B. imba

C. imbisha

D. wimbo

**24.** Ukizidisha robo na nusu utapata akisami ipi?

A. Robo nne

B. Thumni

C. Nusu

D. Subui

**25. Kanusha sentensi hii:-**

Yeye ndiye aliyepika chakula akala.

A. Yeye siye aliyepika chakula wala kukila.

B. Yeye siye asiyepika chakula na kukila.

C. Yeye ndiye asiyepika chakula wala kula.

D. Yeye siye aliyepika chakula wala akala.

**26.** Nomino ***'minana'*** inapatikana katika ngeli ipi?

A. I - I

B. I - ZI

C. A - WA

D. LI - YA

**27.** Chagua jibu lililo na maelezo sahihi

A. Kitalu - Makao ya mfalme

B. Kanda - Mtu aliyepotoka kimaadili

C. Fuma - Sehemu ya kukanyagia ya mnyama

D. Kipaji - Sehemu ya nchi ya kiuno

**28.** Ni sentensi ipi iliyo katika wakati uliopita?

A. Hakufika mkutanoni.

B. Hajafika mkutanoni.

C. Hawatafika mkutanoni.

D. Hufika mkutanoni.

**29.** Salamu ***'alamsiki'*** hutumiwa kuagana wakati wa

A. asubuhi

B. alasiri

C. mchana

D. usiku

**30.** Shairi la mishororo mitatu huitwaje?

A. Takmisa

B. Tathnia

C. Tathlitha

D. Tarbia

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 31 mpaka 40.**

Majuto alijiinamia kama mtoto aliyefiwa. Aliwaza na kuwazua alipokuwa akifanya adhabu aliyopewa na kinara wa shule. Alikumbuka jinsi bangi ilivyombangaisha alipoivuta mara ya kwanza. Alikumbuka jinsi alivyozoeshwa tabia ile na marafiki zake wawili. Alikumbuka jinsi alivyoanza ajabu kila baada ya kuivuta. Wakati mwingine alijikuta akicheka ovyoovyo!. Bila kung'amua, akawa ametumbukia kwenye bahari ya ulevi. **Uraibu** jamani! kuwacha tabia yake hii ikawa ngoma.

Upweke aliokuwa nao alipokuwa akifanya kuwachukia ili ulimzindua. Akili yake ikaamka. Alianza kuwachukia wale marafiki zake waliomshawishi kushiriki ulevi, akawahesabu kama maadui wake. **"Kikulacho ki nguoni mwako,"** tena ni **"nazi mbovu harabu ya nzima."** Alikumbuka maneno haya ya mwalimu wake wa Kiswahili. Alichukia vilevile jinsi nguo yake, vitabu vyake na vitu vingine vyake vilivyonuka sigara. Alichukia jinsi meno yake na vidole vya mikono vilivyogeuka rangi kwa ajili ya sigara alizozitumia. Alijilaumu kwa namna tumbo, kichwa na kifua vilivyokuwa vikimuuma. Akahofu kuwa matumizi ya dawa za kulevya yangemponza.

Tangu alipoanza kuwa mraibu wa vileo, mwili wake ulikuwa umekosa nguvu na kuonekana mnyonge. Akikosa afya na kila wakati alijihisi amechoka tiki. Masomo nayo yalikuwa yameanza kumpiga chenga. Isitoshe, hakuwa na wasaa wa kuoga wala kufua nguo zake. Mwenyewe hakujali usafi. Alinuka mff.

Hatimaye, pesa za kutia mfukoni nazo alizikosa kabisa. Masurufu aliyokuwa akipewa alitumia ndivyo sivyo akawa na **mkono mrefu**. Aliuzauza vitu muhimu vya nyumbani na hata vitabu vyake ili kujitosheleza.

Majuto tayari alikuwa ameanza kuwa tishio hata kwa wanafunzi wenzake. Alitumiwa na walanguzi wa dawa za kulevya kutimiza ndoto zao. Alipotambua kuwa yeye hakupenda kuwa mwizi wala kuhusishwa na wizi, machozi yalimlengalenga machoni. **"Sitatumia vileo vya namna yoyote tena.** Tamko hili alilolitamka kwa sauti kuu ndilo lililomfanya kinara wa shule Bw. Busara kumsamehe na kumnasihi Majuto.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**31.** Ni wazi kusema kuwa

A. Majuto alizoea kuadhibiwa shuleni.

B. Majuto alikuwa amefiwa.

C. Majuto alihisi vizuri alipovuta bangi.

D. Majuto alishawishiwa na marafiki kuvuta bangi.

**32.** Maana ya neno ***"uraibu"*** lilivyotumika katika aya ya kwanza hasa ni

A. mazoea

B. tabia

C. ujinga

D. ujuaji

**33.** Kwa nini ulevi unalinganishwa na bahari?

A. Ulevi hauna mwisho

B. Si rahisi kutoka ulevini mtu anapozama

C. Vileo vina maajabu mengi

D. Vileo ni vingi na vina madhara mengi

**34.** Kikulacho ki nguoni mwako ni methali. Ina maana kuwa

A. nazi mbovu harabu ya nzima

B. tusivae nguo chafu

C. anayeweza kukudhuru ni mwandani wako

D. adui mpende

**35.** Kwa nini Majuto alianza kuwachukia marafiki zake waliomshawishi kushiriki ulevi?

A. Alifanya adhabu

B. Nguo zake zilinuka

C. Kifua kilimuuma

D. Fahamu zake zilimrudia

**36.** Dawa za kulevya kwa jina jingine zinajulikana kama

A. pombe

B. ugoro

C. madawa

D. mihadarati

**37.** Alikosa afya na kila wakati alijihisi amechoka tiki. Ni tamathali gani ya lugha iliyotumika katika sentensi hii?

A. Tanakali za sauti

B. Tashbihi

C. Takriri

D. Isitiara

**38.** Majuto angeuchukia uchafu na kuupendelea usafi basi tungesema yeye ni

A. msafi

B. safi

C. msifa

D. sawa

**39.** Je, ni kweli kusema kuwa

A. Majuto hakujuta

B. Mwalimu mkuu alimsamehe Majuto

C. Majuto alishindwa kusoma

D. Majuto alikuwa nadhifu

**40.** *"Sitatumia vileo vya namna yoyote tena,"* ni maneno ambayo Majuto

A. aliwaambia watu wote

B. alimwambia mwalimu mkuu

C. aliiambia nafsi yake

D. aliwaambia walanguzi

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50**

Kusema yakini, miti ina manufaa chungu nzima. Ningeulizwa mimi binafsi, ningekiri dhahiri shahiri kuwa pengine kama binadamu walipendwa sana na Maulana, basi miti ni nambari ya pili kupendwa na yuyo huyo muumba.

Tafakari jinsi maua hutokezea na kunawiri. Urembo una ulimbo. Upitapo karibu na mimea yenye maua wewe hujihisi vipi hasa? Nilistaajabu ya Musa nilipogundua kuwa mmea unaozaa mawaridi huwa na miba si kichele! Basi wewe unayeyapenda mawaridi,fahamu fika kuwa mmea duni waweza kutupatia zao zuri.

Vile vile, mandhari yetu nayo yameungwa na kufanyika mazingira bora kwa miti. Hewa safi, vivuli na hata mielekezo huwa kazi ya miti. Utampata insi akitembea astaaste kuelekea ofisi fulani, huku kiongozi au mwelekezi wake ikiwa tu mimea iliyopangika vilivyo kando kando ya barabara.

Fauka ya hayo, hebu tutazama sote kule. Nasema kule hadi upeo wa macho. Endapo utaweza kuangalia kusini au kaskazini na uufikie utaweza kuangalia kusini au kaskazini na uufikie upeo wa macho yako bila kuona mimea au miti fulani, basi kuna kasoro. Sehemu kama hiyo huwa na uhaba wa mvua. Tusijenge mijengo mingi tu tukisahau kuiwachia mimea sehemu za kuota. Kumbuka kuwa mimea midogo midogo haikuombi mambo mengi ili kujiotea inavyokuwa desturi yake.

Hivi maajuzi sote tumeshuhudia mabadiliko katika hali ya anga. Mvua imekunya udongo ukasirima. Mafuriko yakaleta majanga. Sauti za mahaluki zikaenea kote, si runingani, redioni, mitandaoni na magazetini. Eti mvua hiyo ya majanga ilitokea katika nchi jirani!

Jamani! Fanya busara ya kupanda miti mingine mingi kuongeza misitu kabla kujaribu kukata japo mmoja. Zingatia wito wa wanamazingira. Nchi yetu inaelekea kugeuka jangwa kutokana na ukatili wetu wa kutopenda miti. Shime! Tupande miti.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza

A. Miti ina faida kiasi

B. Miti ina umuhimu mwingi

C. Mimea inaweza kujaa chungu

D. Mimea ina manufaa ya kujaa chungu

**42.** Katika aya ya kwanza, maneno ***'yuyo huyo'*** yametumika. Je, maneno haya ni aina ipi ya viashiria?

A. Viashiria visisitizi

B. Viashiria radidi

C. Viashiria viulizi

D. Viashiria kamili

**43.** Kamilisha methali:-

Ukistaajabu ya Musa

A. utayaona ya miti

B. utayaona ya Firauni

C. utapata ya maua

D. utapata ya misitu

**44.** Je, maneno ***'mmea'*** na ***'mti'*** hupatikana katika ngeli ipi?

A. I - ZI

B. U - ZI

C. U - I

D. U - U

**45.** Kwa nini mwandishi anasema kuwa ***'tutazame kule hadi upeo wa macho"?***

A. Ili tuone jua likizama

B. Ili tupande mimea

C. Ili tufurahie mazingira yenye mimea

D. Ili tuweze kukadiria kuwepo kwa miti

**46.** Ni hali ipi kati ya hizi haisababishwi na uhaba wa mvua?

A. Mafuriko

B. Ukame

C. Jangwa

D. Kiangazi

**47.** Mimea midogo midogo ambayo mara nyingi huota kutoka kwenye mbegu huitwa

A. michi

B. maua

C. miti

D. miche

**48.** Je, unafikiri ni kwa nini mwandishi hajaridhia sauti za mahuluku zilizotokea vyombo vya habari?

A. Zilitangaza uongo

B. Sauti hizo hazikufaa vyomboni

C. Ujumbe wa sauti hizo ulimshangaza

D. Mvua haiwezi kutoka nchi nyingine

**49.** Mafuriko yawezeza kusababisha haya yote ila

A. kuua watu na wanyama

B. kusomba hewa

C. kubomoa nyumba

D. kumomonya udongo

**50.** Mada mwafaka ya kuipa taarifa hii ni ipi?

A. Faida za miti

B. Miti ni mambari ya pili

C. Tupande miti

D. Mazingira